# Taasisi ya Thirdmill

## Beji ya jinsi ya Kufundisha/Kuhubiri

*Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika Maandiko Matakatifu kuanzia Musa hadi manabii wote.*
Luka 24:27

Kufafanua kwa uaminifu na kwa usahihi ujumbe wa Biblia ni kazi ngumu. Ikiwa ni kufundisha mbele ya darasa au kuhubiri katika mimbari, watu wanahitaji kupata picha halisi ya ujumbe wa Biblia kuhusu mada mbalimbali. Yesu akiwa njiani kuelekea Dameski, alitumia muda huo kuwaelezea wanafunzi wake kuwa yeye alikuwa nani. Beji hii imejikita katika lengo hili mahususi. Wewe pamoja na mkufunzi wako kama mwezeshaji, kwa pamoja mtajifunza ili kuendeleza na kujenga ujuzi katika kufundisha na kuhubiri ili muweze kuhubiri Maandiko kwa uaminifu

## Vipengele vya Beji:

**Uaminifu kwa Kifungu** – Sema kile ambacho kifungu kinavyosema
**Uaminifu kwa kifungu kidogo** – Ni kwa jinsi gani somo lako/mahubiri yako yanamwelezea Yesu na kazi yake?
**Uaminifu kwa Muktadha** – Husianisha ulimwengu wa Kibiblia na ulimwengu wako kwa njia ambayo inaeleweka kwa hadhira yako.

## Mada za Kujadili:

**Vitendo** – Mafundisho au mahubiri yakoje kwenye kanisa au huduma yako? Ni nani ambaye mara zote anahubiri au kufundisha? Je, anatumia muda gani kufanya hivyo?

**Maombi** – Nafasi ya maombi ni ipi katika kuchagua kifungu, kuandaa somo au mahubiri, kuwasilisha, na kumtegemea Roho Mtakatifu kwajili ya matokeo?

**Mpango** – Ni jinsi gani unapaswa kuchagua kifungu au mada? Ni kifungu gani cha Maandiko kinahusiana na mada unayotaka kufundisha?

**Mgawanyo** – Kifungu kimegawanywa vipi? Mada ya kifungu hicho ni ipi? Somo kuu la kifungu hicho ni lipi? Ni mada zipi ndogo ambavyo mwandishi ametumia kuelezea somo kuu? Ni vielelezo gani vimetumika kufafanua somo?

**Jiandae** – Je, kuna maneno au sentensi za kutatanisha katika kifungu husika? Je, kuna majina au sehemu za muhimu ambazo zinapaswa kufafanuliwa? Je, unahitaji nyenzo gani ili zikusaidie kujifunza kifungu husika? Ni jinsi gani mwandishi huyu au waandishi wengine wa Biblia wanaelezea mada husika?

**Watu** – Ni watu wa hulka gani waliopo kwenye eneo au kikundi ambacho unahubiri kufundisha?

**Lengo** – Ni matokeo ya aina gani unatarajia kutokana na mazungumzo yako?

**Pogoa** – Ni mifano au mawazo gani yanafaa kutunza? Na yapi ya kuondoa?

**Zalisha** – Je, unapaswa kuandika somo au mahubiri yako na kisha kuyasoma mbele ya wasikilizaji wako? Au uandike na kisha kukariri? Au uwe na muhtasari na nukuu fupi kwaajili yako?

**Fanya Mazoezi** – Je, ni muhimu na ni wapi unapaswa kufanyia mazoezi somo au mahubiri yako kabla ya kuyawasilisha? Na baada ya kufanyia mazoezi, kuna jambo unapaswa kubadilisha?

**Onyesha** – Katika Luka 24:27 Yesu alipokuwa njiani kuelekea Dameski, alifundisha jinsi ambavyo Maandiko Matakatifu yanamtabiri yeye. Ni kwa jinsi gani somo au mahubiri yako yanamlenga Yesu?

**Kasi** – Je, unaongea haraka sana, au polepole sana, au pasipo mabadiliko kasi ya kuzungumza?

**Kutoa** – Umewapata wasikilizaji wako kitu cha kutafakari au kufanyia kazi wanapoondoka?

**Tafakari** – Je, hadhira yako itatiwa nguvu katika upendo wao na kujitoa kwao kwajili ya Yesu pekee?

**Nguvu** – Kuna tofauti gani katika kufundisha au kuhubiri kwa kuongozwa na nguvu ya Roho Mtakatifu na kufanya hivyo kwa nguvu zako mwenyewe?

## Mambo ya Kufanya:

1. Kwa kufuata hatua zote kama ulivyoelezwa na mkufunzi wako, andaa somo/mahubiri na kisha ufundishe au kuhubiri kwenye kikundi chako.

2. Uliza maswali yafuatayo kwaajili ya kupata mrejesho: Kitu gani kimeeleka zaidi? Kitu gani hakikueleweka? Ni kitu gani kimekugusa wewe binafsi?
Mawazo haya yataleta tofauti gani kwenye maisha yangu?
Je, somo hili au mahubiri haya yameongeza shauku yangu yangu ya kumpenda Yesu?

3. Wasilisha somo/mahubiri haya pia kanisani kwako

## Vigezo vya Beji:

Utatunukiwa Beji hii na tasisi ya Thirdmill kama sehemu ya Cheti cha Misingi baada ya kufuzu vigezo vyote vya Beji vilivyo kwenye ***mambo ya kufanya*** kwa uaminifu, na ***uthabiti,*** *na* kwa kufuata ***vipengele vya Beji*** na muktadha wa ***mada zilizozungumziwa*** katika kipindi chote cha kozi.